

SIRI JUU YA ISRAELI YA KIROHO YA KIBIBLIA

“Kwa maana, ndugu zangu, sipendi msijue siri hii, ili msijione ua wenye akili; ya kwamba kwa sehemu ugumu umewapata Israeli, mpaka utimilifu wa mataifa uwasili. Hivyo Israeli wote wataokoka.” (Warumi 11:25-26)

Sikilizeni kile nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo:

Biblia ilisema, “Israeli wote wataokolewa.” Sasa, “Israeli si Israeli ambayo ni ya kimwili, bali ni Israeli ya Roho, kwa kuwa karama na miito havina majuto.” (Warumi 9:6-13; 11:29) Je! hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa? Vema. “Israeli wote wataokolewa. Kila mmoja wao ameokolewa.” Tunakuwaje Israeli? “Tukiwa wafu katika Kristo, tunakuwa Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi kulingana na ahadi.” (Wagalatia 3:29).

Paulo alisema, “Kile kilicho kwa nje si Myahudi, bali ni kile kilicho moyoni, ndicho kilicho Myahudi, Wale walioahidiwa.” Nasi ni Mzao wa Ibrahimu, kwa ile ahadi, kwa njia ya Kristo, tulimkubali Yeye kama Mwokozi wetu binafsi (Warumi 2:28-29). [1]

Ndugu Branham anapitia Warumi 11:25-32 na Wagalatia 3:27-29 na kuonyesha hasa mstari 29: “Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekua uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi”

Tena tunasoma katika Warumi 2:28-29, “Maana yeye si Myahudi kwa nje tu, wala tohara siyo ile ya nje tu katika mwili; Bali yeye ni myahudi aliye myahudi kwa ndani, na tohara ni moyo, katika roho, si katika andiko; ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu.”

Tafadhali soma pia katika Matendo 7:51, na hasa Wafilipi 3:3,

“Maana sisi tu tohara, tumuabuduo Mungu kwa Roho, na kuona Fahari juu ya Kristo Yesu, wala hatuutumaini mwili.”

Neno la Kiyunani, *Kumbukumbu la Torati*, linamaanisha “sheria mbili mbalimbali.” Na hizo ndizo tu Mungu alizo nazo, sheria mbili mbalimbali. Na mojawapo ni sheria ya mauti, na nyingine ni sheria ya Uzima. Mungu ana sheria mbili. Kumfuata Yeye, na kumtumikia na kumwabudu Yeye, ni Uzima; kukataa jambo Hilo ni mauti. Kuna sheria mbili ndani ya Mungu.

Sasa, mojawapo ya sheria hizo ilitambu... ilitambuliwa na ulimwengu, katika Mlima Sinai. Mungu alimpa Musa na Israeli sheria (Kutoka 19). Siyo kwamba ile sheria ingeweza kuwasaidia, bali ile sheria iliwaonyesha kwamba walikuwa wenye dhambi (Warumi 7:7-25). Hadi wakati ule, hawakujua dhambi ilikuwa ni nini, mpaka walipopata sheria. Hapawezi

kuwa na sheria bila ya adhabu. Sheria si sheria, bila ya adhabu. Kwa hiyo, basi, “Kuvunja sheria ni dhambi, na mshahara wa dhambi ni mauti(Warumi 6:23).” Kwa hiyo basi, hadi Mungu alipowafanyia sheria, hawakuhesabiwa makosa.Kama hakuna sheria hapa ambayo inasema huwezi kwenda zaidi ya maili ishirini kwa saa, basi unaweza kwenda zaidi ya maili ishirini kwa saa. Lakini ikiwepo sheria isemayo huwezi kufanya hivyo, basi kuna sheria na adhabu nyuma yake.

Sasa, mauti, sheria ya mauti, ilikuwa ni zile amri zilizotolewa katika Mlima Sinai, ambazo zilimwambia binadamu kwamba alikuwa mwenye dhambi. Na, kuzivunja sheria za Mungu, alikufa. Bali hakuna wokovu katika torati. Ile...Ilikuwa ni polisi tu ambaye aliweza kukufunga jela; haikuwa na kitu cha kukufungulia.Lakini basi Yeye alitoa sheria nyingine, hiyo ilikuwa katika Mlima wa Kalvari, ambako dhambi ilihesabiwa katika Yesu Kristo, na hapo adhabu ikalipiwa. Na sio na...Bila ya sheria, “lakini kwa neema umeokolewa,” kwa neema ya Mungu, kwa kuchaguliwa hapo awali kwa ajili ya Mungu kukujua tangu awali(Waefeso 2:8-10).

Sasa tunaona sheria hizi mbili, Kumbukumbu la Torati, ikizungumzia juu ya sheria mbili. Kulikuwa na sheria mbili. Moja ilikuwa sheria ya mauti, na ile nyingine sheria ya Uzima.

Kulikuwa pia na maagano mawili waliyopewa watu. Tutayazungumzia asubuhi.Moja lilitolewa kwa Adamu kwa masharti, “ukitenda *hili* na usitende *lile*,” lakini sheria hiyo ilivunjwa. Adamu, Hawa aliivunja hiyo, katika bustani ya Edeni(Mwanzo 3:1-13).Halafu Mungu akafanya agano la pili, na akampa Ibrahimu hilo, na sheria hiyo ilikuwa bila masharti. “Si kile ambacho umetenda au kile utakachotenda;” Yeye alisema, “Nimekwisha litenda.”(Mwanzo 13:14-18) Hiyo ni neema. Hiyo ni sheria ya Uzima(Warumi 8:1-2). Mungu alitenda jambo hilo kwa ajili ya Ibrahimu na Uzao wake baada yake, hiyo ni kusema, Uzao wote wa Ibrahimu.Kama Biblia ilivyosema, “Israeli wote wataokoka,” lakini hiyo haimaanishi Wayahudi. Kama Paulo alivyosema, “Aliye Israeli kwa ndani, au Israeli kwa nje.” “Kwa nje,” kama tulivyolizungumzia usiku wa juzi, ilikuwa ni watoto wa Isaka, kwa kujuana kimwili. Lakini sheria ya Mungu ilikuwa kwa njia ya Kristo, ambaye alikuwa Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, kwamba, “kwa neema Israeli wote wapate kuokoka.” Hiyo ni kusema, “Wote walio katika Kristo wameokoka,” wote, agano la pili la Mungu. Bali mambo haya yote yalikuwa kivuli cha Kristo. [2]

Swali: Je! ni kweli ya kwamba kila Myahudi aliyezaliwa tangu Kristo, alipokuja ulimwenguni, ataokolewa?

La. Hakuna watakaokolewa, ila wale tu ambao majina yao yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, Myahudi ama Mmataifa. Unaona? Hivyo tu. Kitabu hicho kinashikilia siri hiyo, na Kitabu hicho kinaifungua tu hivi sasa; si jina la kila mtu, lakini kwamba siri ya Kitabu hicho ni, wakati inapoyaita majina hayo. Hatimaye mnafahamu jambo hilo sasa?

Kitabu hicho hakisemi, “Sasa, Lee Vayle ataokolewa katika kipindi cha wakati huu wa kanisa, ama Orman Neville...,” ama ye yote yule. La, hakisemi hivyo. Kinaonyesha tu ile siri, kinafungua tu siri ya kwamba kitu hicho ni nini. Lakini sisi, wenyewe, kwa imani, tunaamini jambo Hilo. Hivyo ndivyo nilivyosema hivi majuzi.

Mtu fulani alisema, “Vema, hakuna haja ya mimi kujitahidi. Ndugu Branham alisema kutakuwa na mmoja tu atakayeokolewa kutoka Jeffersonville.” Mnaona? Sasa, mnaona, ni ku onyesha mfano. Hivyo sivyo, hivyo sivyo hivyo. Huenda maelfu wakaokolewa. Sijui. Natumaini kila mmoja wao ameokoka, unaona, lakini sijui.Lakini nataka kuamini jambo hilo kwa namna hii

hapa, “Huyo mmoja ni mimi.” Wewe amini vivyo hivyo kwa ajili yako. Usipoamini hivyo, basi kuna kasoro katika imani yako; huna hakika ya kile unachofanya.

Wawezaje uende pale mbele ya mauti, wakati huna hakika mno kabisa kama umeokoka ama hujaokoka? Unaona? Wawezaje kwenda hapa na kumwambia huyu mwanamume kilema anayelala hapa, amepofuka na amelemaa, “BWANA ASEMA HIVI. Amka! Yesu Kristo anakuponya”? Wawezaje kustahimili, maskini mwili huo baridi na mkavu uliolala pale, ambao umekufa, na umekufa kwa masaa kadha wa kadha, na umelala pale, na uko pale, wenye baridi na ni mkavu; na useme, “BWANA ASEMA HIVI, simama kwa miguu yako”? Heri, heri ujue unachoonea. Unaona?

Vema, wasema, “Mauti huchukua kila kitu. Yote yamekwisha.” Naam, lakini Neno la Mungu linapofunuliwa, na unajua ni Mungu, hilo hubadilisha mambo. Hiyo ni kweli. Sasa, naam, hawa Wayahudi si wote wataokolewa. La, bwana. Hawataokolewa; ila wale tu ambao...

Yeye anaponena kuhusu Myahudi, “Mayahudi,” ni jina tu walilopewa baada ya kuondoka...Naamini, Nebukadreza, kule, ndiye aliyeanza kuwaita ni “Wayahudi,” kwanza, kwa sababu lile kabila la Yuda lilichukuliwa kule. Nao wakapewa jina la “Myahudi,” sasa, kwa sababu walitoka Yuda, nao wakapata jina la Myahudi. Lakini sasa, Israeli ni kitu tofauti. Israeli, na Myahudi, ni vitu tofauti kabisa kabisa. Kila Myahudi si Mwisraeli, unaona. La, yeye ni Myahudi tu. Lakini, basi, Israeli...Paulo hakusema Wayahudi wote wataokolewa. Alisema, “Israeli wote wataokolewa.” Kwa nini? Jina la Israeli, hilo ni jina la ukombozi, kutoka huko nyuma kote. Unaona? Na Israeli wote wataokolewa, lakini si Uyahudi yote.

Kama vile tu Mataifa, kutakuwa na maelfu mara maelfu ya watu, naam, mamilioni kabisa, katika madhehebu haya, na yanaitwa “ya Kikristo, kanisa la Kristo,” na majina yote kama hayo. Hayo hayamaanishi cho chote. Hiyo haimaanishi wataokolewa. Watu husema, “Sasa, yabidi uwe katika *hili* ama *lile*, madhehebu, madhehebu fulani. Kama jina lako halimo katika kitabu chetu, umepotea.” Sasa, hilo ni kundi lililojitenga. Unaona? Hilo ni kundi lililojitenga. Kuna njia moja pekee uwezayo kuokolewa, na, hiyo ni, “Si katika uwezo wa yeye atakaye, wala yule apigaye mbio, Basi, ni Mungu arehemuye.(Warumi 9:14-23)” [3]

Lakini njia pekee ninyi mmeokolewa, ni kwa mjua Yeye kwa Ufunuo! Kanisa lake ni yeye mwenyewe akifunuliwa. Kwa ufunuo kwamba Mungu amefunua Neno kwako! Yeye ni Neno. Unajuaje limefunuliwa? Litaishi lenyewe na kujidhihirisha lenyewe kupitia wewe. [4]

Naye Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alichagua Kanisa kwa ajili ya Utukufu Wake, na hao ndio wanaokolewa. Kweli. Sasa, imani yako imetiwa nanga sana Hapo!

Unasema, “Vema, imani yangu imetiwa nanga Huko.” Na basi angalia unaishi maisha ya namna gani. Unaona hata hustahili kuwa Huko. Nanga yako imetiwa mahali pabaya. Umeitia kwenye changarawe badala ya kuitia kwenye mwamba. Wimbi dogo la kwanza litaing’oa.

Hebu Neno lifunuliwe katika kitu fulani. “Kanisa langu halifundishi jambo Hilo!” Hiyo inaonyesha papo hapo wewe hukuwa umetiwa nanga kwenye mwamba wo wote. Wewe ulikuwa kwenye mchanga.(Mathayo 7:24-27; 16:13-19).

Sasa, **Na wale 144,000, je! hao ni wale waliochaguliwa tangu zamani?** Naam, bwana. Hao ni Israeli, Israeli wa kiroho. Hebu fikiria tu, kutakuwako na mamilioni yao humo. Sijui ni wangapi walioko humo sasa; Nadhani ni kundi lote, lakini si wote wataokolewa ati kwa sababu wako Uyahudi. Mnaona?

Hivyo basi, angalieni hili:144,000—Ni wale waliochaguliwa kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu?(Ufunuo 7:2-8)- Ndio bwana, hiyoni sahihi kabisa! Sasa, Kama sikulijibu, kukuridhisha, mbona, labda mimi ni...Ningeweza kukosea, unaona. Lakini, haya, ndiyo yote kabisa nijuayo mimi, mnaona. Haya ni kadiri nijuavyo mimi kabisa. [3]

Hii hapa tena:Uzao wa Ibrahimu ni upi? - Sisi ni uzao wa Ibrahimu, kwa kuwa sisi tu wafu katika Kristo, ndivyo tulivyo, tunafanyika uzao wa Ibrahimu nasi tu warithi pamoja naye chini ya ahadi ile ile iliyoapiwa. Sisi tu uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi wa kila ahadi aliyopewa. Lakini, majaribio yajapo, hapo ndipo tunaposhindiwa. Bali siamini ya kwamba uzao wa kweli wa Ibrahimu utashindwa, wao watasimama kwa ushujaa na uaminifu kama alivyofanya Ibrahimu.

Wanadamu sio wasiokosa, bali Mungu hakosei. Mwanadamu, ukiweka nia yako juu ya mwanadamu, yeye atafanya kosa. Labda si kwa kupenda, bali yeye atafanya hivyo. Mungu humruhusu afanye hivyo kusudi aitikise imani yako itoke kwa mwanadamu. Imani yetu haimo katika hekima ya mwanadamu, bali katika nguvu za ule ufufuo wa Yesu Kristo. Hapo ndipo ule uzao halisi wa Ibrahimu hupumzisha ahadi yao, kwa sababu wao wanaweza tu kuwa uzao wa Ibrahimu wanapompokea Roho Mtakatifu(1 Wakorintho 12:13). Bila Roho Mtakatifu wao si uzao wa Ibrahimu. Na imani ile ile iliyokuwa katika Ibrahimu humjia mwamini(Wagalatia 3:9). Haidhuru nini kitakachotendeka au ni kinyume vipi, mwamini husonga mbele moja kwa moja. [5]

Siri ni maandiko,ukweli uliofichwa hapo kwanza, sasa umefunuliwa Kiungu, bali bado pamebakia jambo la kimbinguni, hata ingawa limefunuliwa. Siri zilizo Kuu zaidi na Siri Kuu ni:.....Siri ya 4, ya Kanisa la Agano Jipya kama Mwili Mmoja, Uliofanyizwa kwa Wayahudi na Mataifa. (Waefeso 3:1-11, Warumi 16:25, na pia Waefeso 6:19, Wakolosai 4:3).[6]

Wagalatia 6:15-16, “ Kwamaana kutahiriwa sio kitu, wala kutokutahiriwa, bali kiumbe kipya. Na wote watakaoenenda kwa kanuni hiyo, amani naiwe kwao na rehema, naam, kwa Israeli wa Mungu. ”

Nukuu:

[1] “Waebrania sura ya 6, Sehemu ya2”(57-0908E) Aya, 437-438

[2] “Mahali pa kuabudia alipochagua Mungu” (65-0220), Aya 21-25

[3] “Maswali na Majibu juu ya muhuri” (63-0324) Aya, 113-125

[4] “Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa” (63-0728), Aya 250,252,255

[5] “Kumiliki malango ya adui” (59-1108), Aya 18+35

[6] “Je hii ndio Ishara ya mwisho Bwana” (62-1230E), Aya 244,248

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Joseph C Kanju

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: kanjuseph23@gmail.com

Cellphone: 0654335361